HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE

05-06/11/2017

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Mhe. Juma A. Kimisha - Diwani Kata ya Nyamilangano- **Mwenyekiti**
2. Mhe.Gagi Lala Gagi - Diwani Kata ya Igwamanoni – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Tabu R. Katoto - Diwani Kata ya Igunda
4. Mhe.Yohana E. Mange - Diwani Kata ya Mapamba
5. Mhe.Emmanuel N. Makashi - Diwani Kata ya Sabasabini
6. Mhe. Mabala K. Mlolwa - Diwani Kata ya Chona
7. Mhe.Yuda L. Majonjos - Diwani Kata ya Idahina
8. Mhe.Mkomba P. Daudi - Diwani Kata ya Ukune
9. Mhe.Kulwa D. Shoto - Diwani Kata ya Bukomela
10. Mhe.Bundala J. Christopher - Diwani Kata ya Uyogo
11. Mhe.Benedicto A. Mabuga - Diwani Kata ya Mpunze
12. Mhe. Pili E. Sonje - Diwani Kata ya Ushetu
13. Mhe. Sharifu A. Samwel - Diwani Kata ya Kinamapula
14. Mhe.Paschal N. Mayengo - Diwani Kata ya Ulowa
15. Mhe. Doa M. Limbu - Diwani Kata ya Nyankende
16. Mhe.Kulwa E. Mabula - Diwani Kata ya Ulewe
17. Mhe.Damas J. Njige - Diwani Kata ya Chambo
18. Mhe. Hamis M. Majogoro - Diwani Kata ya Ubagwe
19. Mhe.Joseph M. Masaluta - Diwani Kata ya Bulungwa
20. Mhe. Golani P. Sayi - Diwani Kata ya Kisuke
21. Mhe. Gabriela A. Kimaro - Diwani Viti Maalum
22. Mhe.Bernadetha M.Jumanne - Diwani Viti Maalum
23. Mhe.Mary I. Lundalila - Diwani Viti Maalum
24. Mhe. Bether L. Bugaywa - Diwani Viti Maalum
25. Mhe. Esther M. Imambo - Diwani Viti Maalum
26. Mhe. Felister N. Kabasa - Diwani Viti Maalum
27. Mhe.Eva P. Mkonya - Diwani Viti Maalum
28. Ndg. Michael Matomora - Mkurugenzi Mtendaji (W) – **Katibu**

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

1. Mhe. Elias J. Kwandikwa - Mbunge Jimbo la Ushetu – kwa taarifa

WATAALAM WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Christina Akyoo - Afisa Utumishi (W)
2. Ndg. Gervas Magogozwa - Afisa Utamaduni (W)
3. Ndg. Cosmas Maganga - Kaimu Mweka Hazina (W)
4. Ndg. John J.Kimbawala - Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W)
5. Ndg. Onesmo Benjamin - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
6. Ndg. Anna Ngongi - Afisa Kilimo na Ushirika (W)
7. Ndg. Deus Kakulima - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
8. Ndg. Goodluck Ndunguru - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
9. Ndg. Morgan Mwita - Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI
10. Ndg. Zacharia Ngussa - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
11. Ndg. Juma R. Ngogo - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)
12. Ndg. Mapenzi Mshana - Kaimu Afisa Ushirika (W)
13. Ndg. Selestine Lufundisha - Afisa Biashara (W)
14. Ndg. Godfrey Lwambula - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
15. Ndg. Neuster James - Mwanasheria (W)
16. Ndg. Athanas Lucas - Afisa Usafi na Mazingira (W)
17. Ndg. Tumshukuru C. Mudui - Afisa Tarafa Dakama
18. Ndg. Edith Mpinzile - Afisa Elimu Msingi (W)
19. Ndg. Elinight Mmari - Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi (W)
20. Ndg. Charles Pambe - Mhandisi wa Maji (W)
21. Ndg. Salakana J. Peter - Afisa Tarafa Mweli
22. Ndg. Aston Mnkeni - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
23. Ndg. Daniel E.Mwita - Kaimu Afisa Mipango (W)
24. Ndg. Nicodemus Senguo - Kaimu Mganga Mkuu (W)
25. Ndg. Denis Jamhuri Pius - Mratibu wa TASAF III

WAGENI WAALIKWA WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Alphonce Kasanyi - Kny: Katibu Tawala (M)
2. Ndg. Sp Lusana C.Shigumha - Kny: Mkuu wa Magereza (W)
3. Ndg. Mtua Hassan - Kny: Afisa Usalama (W)
4. Ndg. Frank Elophany - Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto (W)
5. Ndg. Henry Mwala - Afisa Uhamiaji (W)
6. Ndg. Mrisho S. Madudi - Kny: Mshauri wa Mgambo (W)
7. Ndg. Said Nampala - Afisa TAKUKURU
8. Ndg. Salvatory Given - Mwandishi wa Habari - Kahama FM
9. Ndg. Paschal Malulu - Mwandishi wa habari –Mtanzania
10. Ndg. Nyamiti A. Nyamiti - Mwandishi wa habari - Divine FM
11. Ndg. Raymond Mihayo - Mwandishi wa Habari - DailyNews
12. Ndg. Faustine Gimu - Mwandishi wa Habari –Baloha FM
13. Ndg. Alexandarina N. Katabi - Katibu wa Chama cha Mapinduzi (W)
14. Ndg. Thomas Mnyonga - M/kiti wa Chama cha Mapinduzi (W)
15. Ndg. Lucy J.Enock - Katibu UWT (W)

16. Ndg. Julius R.Lugobi - Katibu wa Mbunge
17. Ndg. Fabian M. Kamoga - Afisa Serikali za Mitaa
18. Ndg. Timothy Ndanya - Katibu Tawala (W)
19. Ndg. Shaban Alley - Mwandishi wa habari –Star TV
20. Ndg. Erasmus Luziro - Mwandishi wa habari Kwizera FM

SEKRETARIETI

1. Ndg. Warda Yusuph - Mwandisha wa Vikao (CC)
2. Ndg. Emmanuel Stambuli - Mwandisha wa Vikao (CC)

MUHT NA. BM/29/2017/2018- KUFUNGUA MKUTANO

Katibu aliwakaribisha wajumbe, wataalam, wageni waalikwa na Waandishi wa Habari katika mkutano huo, kisha watu wote walisimama na kuimba wimbo wa Taifa uliofuatiwa na sala iliyoongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu.

Katibu alieleza kuwa Halmashauri imekabiliwa na changamoto ya kukosa soko la tumbaku kutokana na zao hilo kuzalishwa kwa wingi na kupita makisio yaliyowekwa hivyo tumbaku kukosa soko la uhakika.

Alieleza kuwa Halmashauri baada ya kuona changamoto hiyo iliamua kuanzisha mazao mbadala ikiwa ni pamoja na zao la korosho na tayari mbegu zilishaletwa kwa ajili ya zao hilo kutoka kituo cha utafiti Naliendele. Kata zilizopendekezwa kuanzishwa kwa zao hilo ni Mapamba, Ukune, Kisuke naIgunda. Kata hizo zilipendekezwa kwa kuwa hazina uzalishaji wazao la tumbaku. Mapendekezo hayo hayazuii kata nyingine kuanzisha kilimo hicho cha korosho

Baada ya kusema hayo alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, wataalam na wageni waalikwa katika kikao kisha aliunga mkono utangulizi aliotoa Mkurugenzi Mtendaji na kueleza kuwa Halmashauri ya Ushetu ina changamoto nyingi ambapo kupambana na changamoto hizo ili kufanya kazi.

Hata hivyo alieleza kuwa zao la tumbaku kwa mwaka huouzalishaji ulikuwa juu kuliko ilivyokuwa imekadiriwa lakini aliomba Serikali kuangalia suala hilo kutokanana Halmashauri ya Ushetu kutegemea zao hilo kimapato.Aidha aliomba kutumia fursa hiyo kabla ya kufungua mkutano kumtambulisha Mwenyekiti wa chama cha Mapinduzi (W) katika kikao na kumkaribisha kwenye kikao.

Alifungua kikao saa 05:30 asubuhi.

MUHT NA. BM/30/2017/2018 - KURIDHIA AGENDA

Katibu aliwasilisha mapendekezo ya agenda kumi na moja (11) ili zijadiliwe kwenye mkutano huo kama ifuatavyo:-

TAREHE 06/11/2017

1. Kufungua mkutano
2. Kuridhia agenda za mkutano
3. Kusoma na kuthibitisha mihtasari ya vikao:
    - Muhtasari wa Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 15-16/08/2017
    - Muhtasari wa mkutano wa mwaka wa Baraza la Madiwani tarehe 17/08/2017
    - Muhtasari wa Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani kupitia na kujadili Taarifa ya Ufungaji wa Hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/2017 tarehe 28/09/2017
4. Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 15-16/08/2017
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi kinachoishia mwezi Septemba, 2017
6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ngazi ya kata
7. Kusitisha mkutano wa Baraza siku ya kwanza

TAREHE 07/11/2017

8. Kurejea kwa mkutano wa Baraza siku ya pili
9. Maswali ya papo kwa papo
10. Taarifa za Kamati za kudumu za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri katika kipindi cha robo ya kwanza, Julai hadi Septemba, 2017
    a) Kamati ya kudhibiti UKIMWI
    b) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    c) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    d) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango

11. Kufunga mkutano

Wajumbe waliridhia kujadili agenda zote kama zilivyowasilishwa na Katibu.

MUHT NA. BM/31/2017/2018 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA VIKAO

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia mihtasari ifuatayo ya mikutano ya Baraza la madiwani ukurasa kwa ukurasa:

- Muhtasari wa Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 15-16/08/2017
- Muhtasari wa mkutano wa mwaka wa Baraza la Madiwani tarehe 17/08/2017
- Muhtasari wa Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani kupitia na kujadili Taarifa ya Ufungaji wa Hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/2017 tarehe 28/09/2017

Baada ya kupitia, wajumbe waliridhia kuwa mihtasari hiyo ni sahihi, Mwenyekiti na katibu walitia saini kwa ajili ya kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

MUHT NA. BM/32/2017/2018 – YATOKANAYONA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 15-16/08/2017

Majibu ya utekelezaji wa yatokanayo yaliwasilishwa kama ifuatavyo:

Kutoka Muht. Na. BM/59/ 2016/2017 – (a) Kuhusu changamoto ya Watendaji wa Vijiji

Azimio kwamba, Watendaji wa Vijiji 73 waliopo wagawanywe kwa uwiano kwa kila Kata ili kutoa huduma stahiki na kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuhamasisha michango na shughuli za maendeleo.

Utekelezaji, ilielezwa kuwakuna waraka uliopokelewa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji uliokuwa ukiagiza kusitisha mishahara ya watumishi waliokuwawameajiriwa kuanzia mwaka 2000 hadi 2004wasio na sifa za kimuundo na kutolewa kibali mbabala cha kuajiri watendaji 33 kwa ajili ya kufidia nafasi za watendaji waliokuwa wamesitishwa kazi, hivyo baada ya taratibu za ajira zao kukamilika watendaji hao watagawanywa kwa usawa katika kata zote.

Baada ya majibu ya utekelezaji wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Sharifu Samwel alitaka kujua stahiki za watendaji kama vile madai ya uhamisho na likizo ikiwa ni pamoja na hatima ya kazi zao lakini pia stahiki zao walizokuwa wakikatwa na mifuko ya Bima kama NSSF na mifuko mingine.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa madai ya watumishi hao ni madeni hivyo anasubiri kupata muongozo ambao utaeleza hatima ya haki zao baada ya kuomba mwongozo huo TAMISEMI na utakapotolewa watalipwa stahiki zao ikiwa ni pamoja na mafao ya hitimisho la ajira zao kutoka mifuko ya hifadhi za jamii.

Mhe. Yohana Mange alisisitiza kuwa hatua za haraka zifanyike katika kutekeleza suala la ugawaji wa Watendaji wa vijiji kutokana na utendaji kazi kuwa wa shidakatika ngazi za vijiji.

Mwenyekiti alieleza kuwa yale yote yaliyotolewa na kushauriwa yachukuliwe na kufanyiwa kazi pindi Mkurugenzi Mtendaji atakapopata muongozo wa maagizo yaliyotolewa kuhusu stahiki za watendaji hao majibu yatawasilishwa katika kikao.

MUHT NA. BM/33/2017/2018 – TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA MWEZI SEPTEMBA, 2017

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha taarifa hiyo na kueleza kuwa, kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2017 Halmashauri imekusanya na kupokea jumla ya Tshs 1,816,019,574.91 na kutumia jumla ya Tshs 1,583,976,646.29 kutoka mapato ya ndani na ruzuku toka serikali kuu kama ifuatavyo:-

MAPATO	**Makisio 2017/2018**	**Mwezi Septemba 2017**	**Mwezi julai – Septemba 2017**	**Albaki**	**Ufanisi %**
Mapato ya ndani	2,697,998,000.00	103,515,006.09	439,556,662.15	2,258,441,337.85	16
Ruzuku za Idara (OC) & GPG	912,758,000.00	170,531,200.00	189,638,200.00	723,119,800.00	21
Mishahara ya (PE)	17,236,060,000.00	1,126,198,000.00	3,396,073,800.00	13,839,986,200.00	20
Miradi ya maendeleo	7,962,350,849.00	415,775,368.82	589,084,403.82	7,373,266,445.18	7
Jumla	28,809,166,849.00	1,816,019,574.91	4,614,353,065.97	24,194,813,783.03	16
MATUMIZI	**Makisio 2017/2018**	**Mwezi Septemba 2017**	**Mwezi julai – Septemba 2017**	**Albaki**	**Ufanisi %**
Matumizi ya mapato ya ndani	947,599,200.00	114,133,333.60	313,469,241.13	634,129,958.87	33
Ruzuku za Idara(OC)& GPG	912,758,000,00	149,017,200.00	149,017,200.00	763,740,800.00	16
Mishahara(PE)	17,236,060,000.00	1,126,198,000.00	3,396,073,800.00	13,839,986,200.00	20
Wanawake & vijana	236,899,800.00	20,000,000.00	20,000,000.00	216,899,800.00	8
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo mapato ya ndani	1,184,499,000.00	39,803,453.69	47,684,753.69	1,136,814,246.31	4
CHF, NHIF na PAPO KWA PAPO	325,000,000.00			325,000,000.00	0
Fedha toka serikali kuu & wafadhili	7,962,350,849.00	134,824,659.00	604,774,969.00	7,357,575,880.00	8
Jumla kuu	28,805,849.00	1,583,976,646.29	4,053,188,353.82	24,751,978,495.18	0.14

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe walijadili kama ifuatavyo

Mhe. Esther Matone alitaka kujua ni kwanini ukusanyaji wa mapato umeshuka hadi robo ya kwanza (Julai- Septemba) 2017/2018 Halmashauri inakuwa imekusanya 16%.

Mhe. Doa Limbu aliunga mkono hoja hiyo, pia alitaka kujua kuhusu Idara ya Ardhi katika upimaji wa viwanja kwa robo nzima wamekusanya kiasi cha Tsh.700,000

lakini matumizi yao kwa robo hiyo ni Tsh. 4,000,000 alihoji fedha wanazotumia zinakusanywa na idara gani.

kuhusu suala la wanawake, vijana na walemavu yaliwekwa makisio ya Tsh. 236,899,800 kwa mwaka ambapo robo ya kwanza ilitakiwa kutoa fedha 60,000,000 lakini haikutolewa fedha yoyote kwa ajili ya kutekeleza makisio yaliyowekwa.

Aidha alitaka kujua kuhusu posho na gharama za vikao kwa waheshimiwa madiwani makisio yalikuwa 255,080,000.00 na hadi sasa fedha iliyotumika ni 110,224,513.00 ambazo ni asilimi 43.21 kwa robo kwa mwaka mzima itakuwa ni sawa na 172% alitaka kujua sababu ya matumizi hayo kuwa juu kuliko bajeti.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza asilimia ya makusanyo kwa robo ya kwanza kuwa 16% katika kiwango cha ukusanyaji bado Halmashauri imefanya vizuri sababu makusanyo ya ushuru wa tumbaku bado hayajatolewa na yatakapotolewa mapatoyatapanda hata hivyo kwa mwezi Oktoba Halmashauri ya Ushetu ilikusanya zaidi ya milioni 100,000,000 na fedha hiyo itaonekana katika taarifa ya mapato ya mwezi unaofuata.

Kuhusu Idara ya Ardhi ilielezwa kuwa Idara hiyo ilikasimiwa bajeti kubwa zaidi tofauti na ukusanyaji wake hivyomarekebisho yatafanyika kipindi cha mwisho mwa robo ya pili mapitio ya nusu mwaka ya bajeti.

Kuhusu suala la wanawake, Vijana na Walemavu alieleza kuwa taratibu zinaendelea kwa ajili ya kutoa fedha hizo na kwa mwaka huu matarajio ya Halmashauri ni kutoa fedha hizo na kufikisha asilimia 100% kulingana na makusanyo.

Kuhusu gharama za vikao, ilielezwa kuwa wakati wa bajeti iliombwa fedha ya kutosha lakini wakati vifungu viliporejeshwa kifungu hicho kilipewa fedha ambayo ilikuwa chini ya bajeti na hivyo alieleza kuwa ipo haja ya kuomba kuongeza fedha zingine kutokana na fedha zake kuwa chache wakati wa kufanya *reallocation.*

MUHT NA. BM/34/2017/2018 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI NGAZI YA KATA

Taarifa za utekelezaji wa miradi ngazi ya kata za Sabasabini, Kisuke na Bulungwa ziliwasilishwa

Baada ya kuwasilisha taarifa hizo Mhe. Emmanuel Makashi alieleza kuwa ukosefu wa magari kwa Halmashauri unakwamisha juhudi za ufanyaji kazi kwa wananchi,hasa wanapoomba wataalam wa kukagua miradi, wanaambiwa kuwa hakuna usafiri.

Ushauri huo ulipokelewa.

MUHT NA. BM/35/2017/2018 – KUSITISHA MKUTANO WA BARAZA SIKU YA KWANZA TAREHE 06/11/2017

Katibu aliwapongeza wajumbe kwa majadiliano ya agenda za kikao alimkaribisha katibu tawala.
Katibu Tawala (W) alitoa pongezi kwa Waheshimiwa Madiwani kwa ushirikiano waliotoa kwa Mheshimiwa Mbunge hadi kufikia hatua ya kupata unaibu Waziri.

Aidha alieleza kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alitoa katazo la ukataji miti na aliagiza upandaji miti ufanyike katika taasisi zote za Halmashauri na maeneo ya kandokando ya barabara.

Alieleza kuhusu msimu wa kilimo wananchi wasisitizwe akisema na kila kaya ilime angalau ekari 3 za chakula na 3 za biashara, pia alisisitiza kilimo cha zao la pamba.

Alieleza kuwa Mkuu wa Wilaya aliagiza kila Afisa ugani asimamie wananchi kulima kilimo bora. Wanatakiwa kuwazungukia wakulima na kukagua kazi zinazofanyika mashambani na si kukaa ofisini

Pia aliongelea suala la ukusanyaji mapato kuwa mapato yanapokusanywa mwananchi anatakiwa kupewa stakabadhi ili kiasi kilichokusanywa kijulikane.

Katibu Tawala (M) alimpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuendesha kikao kwa kufuata kanuni. Piaalimpongeza Mkurugenzi Mtendaji kwa kuanzisha zao la korosho ambalo baada ya muda mfupi litaleta faida kwa wana Ushetu

Mwenyekiti wa chama (W) Kahama alieleza kuwa amefarijika na uendeshwaji wa Baraza katika kutoa hoja na majibu ya hoja.Aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani kwa kumfanya apate nafasi ya uenyekiti wa chama. Aliwasisitiza wataalam kufanya kazi kwa bidii.

Katibu aliwapongeza wageni waalikwa kwa yale waliyoshauri na baada ya hapo alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kusitisha kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru na kuwapongeza wawakilishi wa Mkuu wa Wilaya,Katibu Tawala (M) na Mwenyekiti wa Chama cha mapinduzi aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki katika kikao na kueleza kuwa yale yote yaliyoelezwa na wageni waalikwa yamepokelewa na watayafanyia kazi. Alieleza kuwa mkutano huo kwa kawaida unafanyika kwa siku mbili na hivyo alisisitiza kuwahi katika kikao cha siku inayofuata tarehe 07/11/2017 alisitisha mkutano saa 08:02 mchana.

MUHT NA. BM/36/2017/2018 – KUREJEA KWA MKUTANO WA BARAZA TAREHE 07/11/2017

Katibu aliwakaribisha wajumbe, wageni waalikwa na wataalam katika kikao na kumkaribisha Mwenyekiti kuongozasala kwa ajili ya mwendelezo wa Mkutano, kisha alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, wageni waalikwa na wataalam katika kikao. Alieleza kuwakikao hicho ni mwendelezo wa kikao cha tarehe 06/11/2017 aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kwa kuongozwa na kanuni watumie umahiri walionao kuendeleza agenda za tarehe 07/11/2017.

Alirejesha kikao saa 10:42 asubuhi.

MUHT NA. BM/37/2017/2018 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO

Mwenyekiti alieleza kuwa hadi mkutano huo unaanza alikuwa hajapokea swali lolote la papo kwa papo. Hivyo aliruhusu ajenda zingine ziendelee.

MUHT NA. BM/38/2017/2018 – TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA, JULAI HADI SEPTEMBA, 2017

Taarifa hizo ziliwasilishwa na wenyeviti wa kamati husika kama ifuatavyo:

1) **KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Mwenyekiti wa kamati wa kudhibiti UKIMWI Mhe. Gagi Lala Gagi, aliwasilisha taarifa ya utekelezaji ya kamati hiyo, iliyowasilishwa katika kikao cha kawaida cha Kamati ya kudhibiti UKIMWI cha tarehe 21/07/2017 ambapo muhtasari wake ulithibitishwa tarehe 18/10/2017 pamoja na taarifa ya utekelezaji katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai hadi Septemba) za kamati mseto ya kudhibiti UKIMWI zilizowasilishwa kwenye kikao cha kawaida cha tarehe 18/10/2017.

Mambo muhimu yaliyokuwa katika taarifa hiyo ni pamoja na;

A) MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 21/07/2017 NA KUTHIBITISHWA TAREHE 18/10/2017

MUHT.NA. UK/04/2017/2018 – YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI CHA TAREHE 21/07/2017 NA MAJIBU YAKE

Kutoka Muht. Na. UK/18/ 2016/2017 – kuhusu fedha za mapato ya ndani katika shughuli za kudhibiti UKIMWI

Azimio kwamba; Kamati ya kudhibiti UKIMWI itakapoenda kutembelea na kuona miradi ya ufugaji wa mbuzi kwa ufadhili wa Shirika la Msalaba Mwekundu, itumie wasaa huo kutembelea miradi/shughuli zinazotekelezwa na vikundi vya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, na Ofisi ya Mkurugenzi itoe fedha ili utekelezaji ufanyike.

Majibu ya utekelezaji yalitolewa kuwa, Azimio halikutekelezwa kwa wakati kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo azimio hilo litatekelezwa endapo fedha za ruzuku ya Serikali Kuu zitaletwa kufidia fedha za mapato ya ndani.

B) MUHT.NA. UK/05/2017/2018 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KUDHIBITI UKIMWI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (APRILI HADI JUNI) 2016/2017

Taarifa hiyo iliwasilishwa na Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI (CHAC) aliwasilisha taarifa hiyo, alieleza kuwa Halmashauri kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa huduma za kukabiliana na VVU/UKIMWI ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI, huduma za wagonjwa wa majumbani, ushauri nasaha na upimaji VVU kwa hiari na huduma ya bure ya dawa za kufubaza virusi ya UKIMWI.alieleza kuwa Juhudi hizo zinalenga kufikia **malengo ya sifuri tatu "Maambukizi Mapya sifuri, Unyanyapaa na Ubaguzi Sifuri na Vifo Vitokanavyo na UKIMWI Sifuri".**

Aidha alieleza kuwa Halmashauri ilipanga kutekeleza shughuli 6 kwa kutumia fedha za Mwitiko wa Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI (NMSF) kwa gharama ya Tshs 1,329,043 na shughuli 2 kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kwa gharama ya Tshs 1,872,793 zilizotarajiwa kutumika. Jumla ya shughuli 6 zilitekelezewa kwa kutumia fedha za NMSF kwa gharama ya Tshs 1,329,043.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa Mhe. Sharifu Samweli alieleza kuwa kamati iliagiza wafadhili waandikiwe barua na kupongezwa kutokana na msaada wanaotoa lakini pia Halmashauri kupitia fedha za mapato ya ndani iangalie namna itakavyosaidia fedha ili kamati hiyo itekeleze shughuli ilizopanga.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa maagizo ya kamati yatatekelezwa, Lakini pia katika robo ya pili Halmashauri itafanya jitihada za kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia wananchi wake.

2. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa kamati Mhe. Paschal N. Mayengo aliwasilisha taarifa ya Kamati kwa kuzingatia taarifa za utekelezaji za kipindi cha robo ya kwanza, Julai hadi Septemba,

2017na muhtasari wa kikao cha tarehe 25/07/2017 uliothibitishwa katika kikao cha tarehe 20/10/2017

Mambo muhimu yaliyokuwa katika taarifa hiyo ni pamoja na :

A) TAARIFA YA KIKAO CHA ROBO YA NNE KILICHOFANYIKA TAREHE 25/07/2017 NA KUTHIBISHWA

MUHT.NA. UUM/04/2017/2018 – YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 25/07/2017

i -Kutoka Muht. Na. UUM/17/2016/2017 Kuhusu Kutembelea msitu wa usumbwa unaopakana na pori la Kigosi

Azimio kwamba:-Mkurugenzi Mtendaji awezeshe wajumbe wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kutembelea Msitu wa Usumbwa ili kuona namna ya kusimamia msitu huo.

Utekelezaji, Ziara ilifanyika tarehe 15/08/2017

ii - Kutoka Muht. Na. UUM/33/2016/2017 Kuhusu bei elekezi ya pembejeo za kilimo

Azimio kwamba:-Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa, ushauri umepokelewa na atafuatilia kujua bei elekezi ya pembejeo za kilimo.

Utekelezaji, Kuhusu bei elekezi ya pembejeo katika msimu wa 2017/2018 ilielezwa kuwa Utaratibu wa kusimamia ununuaji na usambazaji wa pembejeo utafanywa na wazabuni badala ya vyama vya Ushirika na tayari zabuni ya kuwapa watoa huduma ya pembejeo imeshatangazwa na Serikali. Punde watakapopatikana bei elekezi ya pembejeo husika itatangazwa na Serikali.

B) MUHT. NA. UUM/05/2017/2018 – TAARIFA YA UENDESHAJI WA MITAMBO YA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (APRILI HADI JUNI) 2016/2017

Taarifa iliwasilishwa na Katibu wa kamati ndogo ya Uendeshaji wa Mitambo,Ilielezwa kuwa, makusanyo ya mitambo yote mpaka kufikia tarehe 31/06/2017 yalikuwa Tsh. 26,650,000.00 (Millioni Ishirini na Sita Mia Sita Hamsini Elfu Tu). Fedha ambazo zilikusanywa kwa kukodishwa *grader, roller na lowbed* kwa kazi mbalimbali za wakandarasi.
Fedha zilizopatikana ziliainishwa kwa mchanganuo wa

- Lowbed 5,650,000/=

- Roller 6,000,000/=
- Grader 15,000,000/=

Jumla 26,650,000/=

C) MUHT. NA. UUM/06/2017/2018 – MPANGO WA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO AWAMU YA PILI (ASDP II) KUANZIA MWAKA 2017/2018 HADI 2022/2023

Mhe. Mwenyekiti, Ilielezwa kuwa, Mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II) unatarajia kuanza mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2022/2023. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na viwanda nchini ikiwa ni pamoja na chanzo cha chakula na lishe, malighafi za viwanda, ajira kwa watanzania na pato la taifa.

Mazao ya kipaumbele ni mahindi, mpunga, mtama/uwele, mikunde, muhogo, mboga/matunda/viazi, alizeti, pamba, kahawa, sukari, korosho, chai, nyama, maziwa, ngozi, mbuzi na kondoo, kuku, samaki na mwani

Aidha ilielezwa kuwa, malengo ya ASDP II ni kufanya mageuzi ya sekta (Kilimo, Mifugo na Uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya usalama wa chakula, kuongeza kipato kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

D) MUHT. NA. UUM/08/2017/2018 – KUPITIA NA KUJADILI RASIMU ZA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI

Mhe. Mwenyekiti, ziliwasilishwa rasimu za sheria ndogo za Halmashauri na kuelezwa kuwa, lengo ni kuhakikisha shughuli zote zinatekelezwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu zilizowekwa na vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria. Rasimu tatu (3) za sheria ziliwasilishwa kikaoni ambazo ni:

i) Sheria ndogo za Ushuru wa Minada ya Mifugo
ii) Sheria ndogo za ushuru wa mazao
iii) Sheria ndogo za kilimo na usalama wa chakula.

Wajumbe wa kamati walipitia na kuridhia rasimu hiyo ya sheria ndogo
Baada ya taarifa ya kamati kuwasilishwa wajumbe walijadili vipengele vifuatavyo

1. Mitambo/Barabara

Mhe. Esther Matone alishauri matengenezo ya trekta yafanyike na yatakapo kamilika ikodishwe ili Halmashauri ipate mapato, alitoa hoja mbili ambazo ni

i. Kujua utaratibu wa kutengeneza barabara kwa kila kata kilomita “20” za kuunganisha barabara hadi barabara

ii. Kujua ni lini barabara ya Ulewe itatengenezwa ukizingatia kuwa greda ilishapelekwa kutengenezwa lakini ikaharibika na kurudi kwa ajili ya matengenezo tena.

Majibu ya hoja Mkurugenzi Mtendaji alieleza iliundwa kamati inayosimamia mitambo ikiwa ni pamoja na trektahivyokamati itakuwa na utaratibu utakao tumika katika kuendesha mitambo hiyo, mapato ya mitamboyatagawanywa katika makundi manne ambayo ni:-

- Kukuza mtaji wa mitambo
- Matengenezo
- Mapato ya Halmashauri ya Wilaya
- Fedha kwa ajili ya kurejesha fedha iliyotumika kununuliwa mitambo

Kuhusu hoja ya barabara ya Ulewe alieleza kuwa suala hilotayari alishaongea na Naibu Waziri mwenye dhamana na aliahidi kutoa mafuta kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo.

Mhe. Mkomba Daud alieleza kuwa lengo la Waheshimiwa ni kufungua barabara na sio kutengeneza barabara isitoshe pia ili kukabidhi barabara hizo ni lazima ziwe zimefunguliwa hata hivyo wananchi wameshafanya kazi za kuondoa visiki hivyo alitaka kujua ni kwa nini mtambo usiende kufungua barabara hizo.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mhe. Mabala Mlolwa pamoja na Mhe. Paschal Mayengo na kushauri kuwa mpango wa TARURA ni kukabidhiwa barabara ambazo zimefunguliwa na jukumu la kufungua barabara hizo ni la Halmashauri hata hivyo kwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji anafanya kazi kwa kufuata mwongozo aandike barua na kufuatilia majibu ili apate mwongozo unao mwelekeza barabara zinazokabidhiwa TARURAziwe katika kiwango gani.

Mkurugenzi Mtendaji aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kuwasilisha orodha ya barabara zilizopo na zinazopakana na kata jirani,lengo barabara zote zisomeke kwenye mtandao “Drawmas”.lieleza kuwa Halmashauri inakabiliwa na ukosefu wa wataalamu wa barabara ambao watashauri

2. **Kilimo**

Mhe. Ester Matone alieleza kuwa Halmashauri ilikuwa na “*power tiller”* lakini hadi sasa haelewi ziko wapi na zinafanya kazi gani hivyo alitaka kupata ufafanuzi juu ya suala hilo.

Afisa kilimo na Ushirika alieleza kuwa *Power tiller* hizo zilinunuliwa wakati Halmashauri ikiwa ni KAHAMA DC na ziligawanywa kwenye vikundi mbalimbali vya wakulima ambavyo kwa sasa baadhi ya vikundi hivyo haviko ndani ya Halmashauri ya Ushetu. Aliahidi kufuatilia vikundi ambavyo vipo ndani ya Halmashauri ya Ushetu

na vilipewa *power tiller* na kuwasilisha majina na mahali vilipo katika Mkutano wa Baraza utakaofuata.

Mhe. Gabriela Kimaro alitaka kujua katika kipindi cha maandalizi ya kilimo Halmashauri inampago gani wa kupelekea pembejeo za kilimo kwa wakulima ili wapate mbegu, viwadilifu kwa mkopo na baadae watarejesha.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa Halmashauri haina mpango wa kupeleka pembejeo za Kilimo kwa wakulima isipokuwa itasimamia na kufuatilia kwa wazabuni/mashirika ili wakulima wakopeshwe pembejeo.

Mhe. Bertha Bugaywa alitaka kujua Halmashauri mpango gani wa kuwawezesha usafiri maafisa ushirika kufika katika vyama vya msingi kutoa huduma kwa wakulima.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa Halmashauri mpango wa kununua gari la Idara ya Kilimo na Ushirika na tayari imeshaomba kibali cha ununuzi TAMISEMI na katika mpango wa bajeti ya 2017/2018 kuna ununuzi wa magari mawili.

3. Afya

Mhe. Sharifu Samwel alieleza kuwa wataalam wa tiba asili ambao walishalipa fedha kwa ajili ya kupata kibali hawajapata vibali hivyo, alitaka kujua ni lini vibali hivyo vitaletwa. Aliongeza kuwa kumekuwa na tabia za Askari polisi kufika katika maeneo ya vijijini kwenye miji ya wataalam hao wa asili na kuwataka watoe vibali vinavyowaruhusu kufanya kazi hiyo na inapotokea hawana vibali hivyo wanawataka kutoa fedha kama faini, alieleza kuwa askari hao wamekuwa wakiwazungukia wataalam tofauti tofauti na kuwatoza fedha nyingi hali iliyopelekea wananchi kuchoshwa na tabia hiyo. Alitoa maelezo hayo kwa masikitiko makubwa na kueleza kuwa maaskari ni walinzi wa amani na usalama wa raia lakini wao ndio wanaoanzisha kuvunja amani kwa raia na kuleta vurugu. Alitaja majina ya askari hao na kutoa namba za simu ambazo askari hao walitaka watumiwe fedha kupitia namba hizo na kuomba jeshi la Polisi liwachukulie hatua kali za kisheria na kinidhamu maaskari hao.

Waheshimiwa Madiwani walisikitishwa na vitendo hivyo viovu vya jeshi la Polisi Wilaya ya kipolisi Ushetu – Nyamilangano, na kuwaomba kufanya kazi kama jeshi linavyoagiza na si vinginevyo kutokana na malalamiko yanayotolewa na wananchi kuwa mengi. Pia waliomba Mkuu wa Kituo awashughulikie mapema askari waliotajwa.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa kuhusu vibali kwa ajili ya wataalam wa tiba asili alifatilia wizarani na alielezwa kuwa kutokana na mlolongo wa uhitaji wa vibali hivyo kuwa mkubwa kutoka katika maeneo mbalimbali bado suala hilo linashughulikiwa na vitakapokamilika vitatumwa. Pia alieleza kuwa kuhusu suala la askari wanaotishia

amani kwa wananchi atachukua maelezo yote yaliyotolewa na kuyapeleka kwa Maandishi.

Kuhusu bodi za afya, Mhe. Sharifu Samwel alieleza kuwa tangu bodi hizo zilipoundwa upya hakuna taarifa zilizotolewa kwa wajumbe hao, ili kuanza kufanya kazi rasmi na kuna fedha zilizopelekwa katika zahanati ambazo zinahitaji bodi kukaa ili kuzifanyia maamuzi alitaka kujua ni lini bodi hizo zitaanza kufanya kazi.

kuhusu wananchi wanaolipa fedha kwa ajili ya kujiunga kwenye mfuko wa CHF na hawapati kadi hizo mapema kwa ajili ya matibabu alitaka kujua sababu inayosababisha kukosekana kwa kadi hizo.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa utaratibu uliofanyika Kuhusu CHF ni kutoa vitambulisho papo kwa papo pindi fedha inapolipiwa hata hivyo wale wanaohitaji kuhuisha kadi taarifa zao zinatumwa Wizarani kwa ajili ya kuhuisha.

Mhe. Yuda Majonjos alitaka kujua ni kwa nini Idara ya Afya haikutekeleza kazi hata moja ilizowasilisha na wakati mwaka wa fedha 2016/2017 ulipokuwa unaisha kuna fedha ambazo idara ilivuka nazo na haikuzifanyia kazi.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa kama kuna fedha iliyobaki itapita kwenye vikao na majukumu mengine yatakayopangwa yataletwa kwenye vikao

4. Maendeleo ya Jamii

Mhe. Sharifu Samwel alieleza kuwa fedha hizo zinatolewa na hakuna mrejesho hivyo alishauri kama itawezekana ifunguliwe akaunti ya pekee kwa ajili ya kuweka fedha hizo na itakuwa ni rahisi kupata mrejesho kupitia akaunti hiyo na faida inayopatikana kufahamika.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuhusu fedha za mkopo za wanawake, vijana na walemavu kuwa tayari serikali ilishaandaa utaratibu wa fedha hizo ambazo zitakuwa kama SACCOS inayojiendesha yenyewe na utaratibu utakapo kamilika waraka utaletwa katika Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji.

5. Fedha

Mhe. Yuda Majonjos alieleza kuwa fedha za machimbo ya mwabomba tayari zilishaanza kulipwa lakini alitaka kujua ni kwanini baadhi ya makampuni hayajaanza kulipa.

Afisa Biashara alieleza kuwa tayari mapato yalishaanza kutolewa, kiasi cha TSh.3,800,000/= zimekusanywa kwa wachenjuaji ambao walitoa kiwango cha 0.3% kwa Halmashauri. Hata hivyo kuna utaratibu uliowekwa wa kuwarasimisha waanze kijiunga katika vikundi na kupewa TIN namba.

6.Maji

Mhe. Hamis Majogoro alitaka kujua utekelezaji wa miradi ya maji visima virefu kwa Kata ya Mbika na Ulowa ni lini utatekelezeka, pia alihitaji kujua ni vijiji vingapi Halmashauri imepanga vipatiwe visima virefu vya maji.

Mwenyekiti alitaka kujua utaratibu wa maji ya ziwa Victoria uliokuwa umepangwa kufanyika katika Kata 6 na vijiji 36

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa, kata ya Ushetu na Ulowa taratibu za utafiti wa maji unaendelea na katika eneo la Ulowa maji bado hayajapatikana na kijiji mbika yamepatikana lakini si mengi. Pia Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa maandiko mbalimbali yalishaandaliwa mengi kwenda Wizara husika na taratibu bado zinaendelea.

3: KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI

Mwenyekiti wakamati hiyo Mheshimiwa Tabu R.Katoto aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji kwa kuzingatia taarifa za kikao na muhtasari uliothibitishwa kwa kipindi cha robo ya kwanza, Julai hadi Septemba, 2017. Kikao hicho ni;kikao cha kawaida cha mwezi Julai cha kamati ya Elimu, Afya na Maji kilichofanyika tarehe 24/07/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 19/10/2017

Mambo muhimu yaliyowasilishwa ilikuwa ni:

A: MUHT WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MWEZI JULAI KILICHOFANYIKA TAREHE 24/07/2017 NA YATOKANAYO YAKE

Majibu ya utekelezaji wa yatokanayo yaliwasilishwa kama ifuatavyo:

Kutoka Muht. Na. EAM/32/ 2016/2017 – (a) Kuhusu vibali vya waganga wa tiba asili

Azimio kwamba; Mkurugenzi Mtendaji ili kujua usahihi kuhusu sifa za usajili wa waganga wa tiba asili, upatikanaji wa vibali na muda wa matumizi ya vibali hivyo na manufaa ya kujisajili ili katika kikao kijacho awasilishe taarifa kamili.Lengo ni kujua kwa nini waganga wa tiba mbadala waliokwishalipia ada ya usajili hawajapatiwa vibali kwa takribani miaka miwili iliyopita.

Majibu ya utekelezaji yalitolewa katika sehemu tatu;

I. **Sifa za usajili wa waganga wa tiba asili**
   - Asiwe mpiga ramli
   - Awe anatambulika kwa Mtendaji wa Kijiji na Kata

II. **Upatiakanaji wa vibali**
   - Hupatikana Wizara ya Afya (Dar es Salaam) kwa Msajili wa Tiba Asili baada ya kujaza fomu na kulipia Tsh 30,000/= vijijini

Ilielezwa kuwa Hadi kufikia Julai 15, 2017 Halmshauri ilipokea vibali 88 vya waganga wa tiba asili, kati ya hivyo vibali 45 tayari vimeshachukuliwa na wahusika. Mchakato wa kuwatafuta waganga ambao hawajachukua vibali vyao unaendelea kupitia watendaji wa Kata.Vibali vilivyosalia vitawasilishwa Halmashauri mara vitakapokamilika na kutumwa kutoka Wizara ya Afya.

III. Manufaa ya kujisajili

- Kutambulika kwa shughuli zote anazozifanya kisheria kwa kufuata miongozo ya Serikali.

Kuhusu wanafunzi 41 ambao hawajaripoti shule kidato cha kwanza 2017

Azimio kwamba; Halmashauri iweke mikakati na kuanza kuwatafuta wanafunzi 41 ambao taarifa zao hazioneshi kuwa wanasoma shule za Serikali ama shule binafsi na kuhakikisha wanaripoti shule na kuanza masomo.

Majibu ya utekelezaji yalitolewa kuwa; Hatua za kuwatafuta wanafunzi watoro zilifanyika na baadhi waliripoti shule kabla ya tarehe 31 Machi, 2017. Majina ya wanafunzi 41 wasioripoti yaliwasilishwa kwa Mkuu wa Wilaya, Maafisa Tarafa na watendaji wa Kata na vijiji kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria kwa wazazi/ walezi wao.

Kuhusu wajumbe wa kamati ya Mikopo ya Wilaya

Azimio kwamba; Kwa kuwa kumekuwepo madai ya Madiwani wanawake kwamba wanatakiwa kuwa wajumbe katika vikao vya kamati ya Mikopo ya Wilaya lakini Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu imekuwa haiwashirikishi. Afisa Maendeleo ya Jamii aliahidi kuandaa mwongozo unaoonesha wajumbe wa kamati ya Mikopo ya Wilaya ili kila mjumbe aelewe.

Majibu ya utekelezaji yalitolewa kuwa; Ilielezwa kuwa Kulingana na mwongozo wa mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Waheshimiwa Madiwani wanawake siyo wajumbe katika vikao vya kamati ya Mikopo ya Wilaya.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, wajumbe wa kamati hiyo ni**:**

1. Mkurugenzi Mtendaji (W) – Mwenyekiti
2. Afisa Maendeleo ya Jamii (W) – Katibu
3. Mheshimiwa Mbunge
4. Afisa Mipango (W)
5. Afisa Maendeleo ya Jamii (Jinsia)
6. Wawakilishi wawili wa wanawake wa vikundi vya wajasiriamali

Taarifa hiyo ya kamati ya EAM ilijadiliwa na kupokelewa

4. KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO

Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Gagi Lala Gagi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango aliwasilisha taarifa ya kamati. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa kuzingatia taarifa za vikao na mihtasari iliyothibitishwa kwa kipindi cha robo ya kwanza, Julai hadi Septemba, 2017/2018. Vikao hivyo ni:

A. Kikao cha kawaida cha mwezi Julai pamoja na kikao cha robo ya nne (April – Juni) cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 28-29/07/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 25/08/2017
B. Kikao cha kawaida cha mwezi Agosti cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 25/08/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 15/09/2017
C. Kikao cha kawaida cha mwezi Septemba cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 15/09/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 26/10/2017.
D. Kikao Maalum cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 27/09/2017 kujadili Taarifa ya Ufungaji wa Hesabu 2016/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 26/10/2017.

Mambo muhimu katika taarifa hiyo ya kamati yaliyojadiliwa ni pamoja na

1. MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI

Ilielezwa kuwa, Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2017/2018 Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya shilingi 1,816,019,574.91 Shilingi 439,556,662.15 ni fedha za mapato ya ndani sawa na asilimia 16 ya lengo la mwaka 2017/2018 la makisio ya shilingi 2,697,998,000.00

2. VIKAO

A. KIKAOCHA KAWAIDACHA TAREHE 28-29/07/2017

MUHT.NA. FUM/07/2017/2018 - TAARIFA YA BAKAA YA FEDHA ZA MWAKA 2016/2017 KUTUMIKA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Ilielezwa kuwa, akaunti za Halmashauri zinazofanya kazi katika mfumo wa “epicor” ambazo zimebaki na salio ni kama ifuatavyo:-

1. Other Charges Account Tshs. 954,244.56
2. Misc.Deposit Account Tshs. 199,248,907.48
3. NWSDP Cash Account Tshs. 496,890,734.30
4. Personal Emolment Account Tshs. 9,440,849.82
5. Road Fund Account Tshs. 15,115,763.23
6. Education Sector Account Tshs. 343,855. 15
7. Health Sector Account Tshs. 138,486,140.88
8. Development Account Tshs. 1,149,073,182.30

9. Own Source Account Tshs. 19,320,924.98

Aidha akaunti zilizoandaliwa bajeti ya bakaa ya mwaka wa fedha 2016/17 kuingizwa katika mwaka wa fedha 2017/18 ni:-

1. Other Charges Account Tshs. 954,244.56
2. NWSDP Cash Account Tshs. 496,890,734.30
3. Personal Emolment Account Tshs. 9,440,849.82
4. Road Fund Account Tshs. 15,115,763.23
5. Education Sector Account Tshs. 343,855. 15
6. Health Sector Account Tshs. 138,486,140.88
7. Development Account Tshs. 1,149,073,182.30

MUHT.NA. FUM/11/2017/2018 - TAARIFA YA MWENENDO WA KESI HALMASHAURI HADI KUFIKIA JUNI 30, 2017

Ilielezwa kuwa kufikia tarehe 30/06/2017, Halmashauri ilikuwa na kesi sita (6) za madai. Na kesi nne (4) ambazo zipo ngazi ya serikali ya kijiji ambazo zinashughulikiwa na kitengo cha sheria. Hivyo kufanya jumla ya kesi za madai kuwa kumi. Pamoja na idadi hiyo, zipo kesi tatu (3) za jinai ambazo zinahusisha watumishi wa Halmashauri waliotuhumiwa kwa makosa mbalimbali ya jinai ikiwemo wizi wa madawa katika zahanati ya Ulowa, upotevu wa fedha za Halmashauri na upotevu wa kitabu cha kukusanyia mapato kata ya Mpunze. Mchanganuo wa kesi hizo za jinai uko kwenye taasisi zinazoendesha mashtaka hayo na Pindi zitakapo hitimishwa, Halmashauri itapewa taarifa ya mwenendo na hatma ya kesi hizo.

MUHT.NA. FUM/12/2017/2018 - TAARIFA YA MANUNUZI YA BODI YA ZABUNI KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (APRIL – JUNI) 2017

Katika kipindi cha robo ya nne, Bodi ya Zabuni katika shughuli zake za utekelezaji ilifanya manunuzi ya shajala za ofisi, mafuta ya magari, mitambo na pikipiki, matengenezo ya magari, ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa ajili ya zahanati na vituo vya afya, vifaa vya ujenzi wa jengo la ofisi ya muda Nyamilangano na zahanati ya Bukomela.

MUHT.NA. FUM/15/2017/2018 - TATHIMINI YA ZIARA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO TAREHE 26-27/07/2017

Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha na tathmini yake iliyofanyika tarehe 26-27/07/2017 ilihusisha miradi 07 iliyotembelewa. Ambayo ilikuwa ni Matengenezo ya kawaida barabara ya Kisuke-Bunasani 9.5, Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa shule ya msingi Bunasani, Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa sekondari ya Igunda, Matengenezo ya kawaida barabara ya Kalole – Idahina -Mwabomba 19km, Ujenzi wa Ofisi za muda za Halmashauri, Kuona masoko ya pamba, Ujenzi wa mradi wa maji ya bomba na wajumbe walipongeza kwa kazi nzuri zilizofanyika na kuongeza kuwa kazi ambazo hazikukamilika zikamilishwe kulingana na makubaliano.

B: KIKAO CHA KAWAIDACHA TAREHE 25/08/2017

MUHT.NA. FUM/25/2017/2018 - TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA NNE APRILI- JUNI, 2017

Taarifa hiyo ilikuwa na hoja 15 ambapo hoja 10 ni za robo zilizopita ambazo hazikupatiwa majibu yaliyojitosheleza, na hoja 5 ni zile zilizojitokeza kwenye robo ya nne ya April- Juni, 2017. Wajumbe wa Kamati ya Fedha walipitia hoja na majibu ya menejimenti kisha kutoa maoni kwa kila hoja.

MUHT. NA. FUM /26/2017/2018 – KUTHIBITISHA MPANGO WA MANUNUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

Mpango wa manunuzi wa mwaka 2017/2018 uliwasilishwa.

MUHT.NA. FUM/27/2017/2018 - TAARIFA YA BODI YA ZABUNI

Taarifa hiyo iliwasilishwa na kufafanuliwa kuwa, sheria ya manunuzi namba 7 ya mwaka 2011 kifungu cha 60(4) na kanuni zake za mwaka 2013 GN namba 446 kifungu cha 231 (3), kinampa mamlaka Afisa Masuuli kuwasilisha taarifa ya Bodi ya zabuni kwa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kabla ya kutoa tuzo kwa wazabuni walioshinda zabuni hizo.

MUHT. NA. FUM/29/2017/2018 - TAARIFA YA VIJIJI VINAVYONUFAIKA NA MRADI WA REA AWAMU YA TATU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU.

Ilielezwa kuwa, Ofisi ilipokea nakala ya barua kutoka Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) yenye Kumb. Na. SHY/RM/RCRO/14 ya tarehe 03 Julai, 2017 iliyotoa taarifa juu ya vijiji vitakavyopatiwa umeme katika mradi wa REA III. Aidha alifahamisha kuwa kuna vijiji 50 katika Halmashauri ya Ushetu vilivyoidhinishwa katika mradi wa REA III mzunguko wa kwanza.

MUHT.NA.FUM/30/2017/2018 - TAARIFA MBALIMBALI ZA KIUTUMISHI KWA MWEZI JULAI, 2017

Iliwasilishwa taarifa ya idara iliyohusu masuala mbalimbali ya watumishi ikiwa ni pamoja na kuajiri, kupandisha madaraja, kuthibitisha kazini watumishi waliokidhi vigezo vya kuthibitishwa kazini pamoja na kushughulika na masuala yote ya kiutumishi kama kusimamia wajibu na haki za watumishi. Idara ya utumishi pia ina wajibu wa kusimamia Sheria, Taratibu na Kanuni na miongozo yote ya kazi na kuhakikisha kuwa miongozo hiyo inatumika mahali pa kazi ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu pale taratibu hizo zinapo kiukwa. Ni wajibu wa Idara ya Utawala na Utumishi kutunza kumbukumbu zote za watumishi na nyaraka mbalimbali za Halmashauri.

Ilielezwa kuwa watumishi wawili (2) wa Idara ya Utawala na Elimu Msingi walizuiliwa mishahara kutokana na makosa ya Utoro kazini, na mtumishi mmoja (1) wa Idara ya Afya alizuiliwa mshahara kwa kushindwa kuwasilisha cheti cha kidato cha nne kwa ajili ya uhakiki.

Aidha Halmashauri ilifanikiwa kulipa mishahara kiasi cha Tsh.1,131,676,250/= ambapo watumishi 1781 walilipwa Tsh. 1,126,692,900/= kwa Ruzuku toka Serikali Kuu na watumishi 21 kwa gharama ya Tsh. 4,983,350/= wanaolipwa mishahara yao kwa mapato ya ndani, kati yao ni watumishi 17 wa mkataba na watumishi 04 wa ajira ya kudumu.

MUHT.NA.FUM/32/2017/2018 - MAPENDEKEZO YA KUTHIBITISHA WAKUU WA IDARA.

Orodha ya wakuu wa Idara ambao walikuwa wamekidhi vigezo vya kuthibitishwa katika vyeo vyao baada ya kutimiza muda wa majaribio, Idara hizo ni Idara ya Maji, Utawala na kitengo cha TEHAMA.

C: KIKAOCHA KAWAIDACHA TAREHE 15/09/2017

MUHT. NA.FUM/39/2017/2018 - TAARIFA ZA KIUTUMISHI KWA MWEZI AGOSTI, 2017

Iliwasilishwa taarifa ya mwezi na kueleza kuwa, Idara ya Utawala na Utumishi inaratibu masuala mbalimbali yanayohusu watumishi ikiwa ni pamoja na kuajiri, kupandisha madaraja watumishi wenye sifa, na kuthibitisha kazini watumishi waliokidhi vigezo. Idara pia ina wajibu wa kusimamia sheria, kanuni, taratibu na miongozo yote ya kazi na kuhakikisha kuwa inatumika mahala pakazi. Ilielezwa kuwa Idara ina wajibu wa kutunza kumbukumbu za ofisi na nyaraka mbalimbali za watumishi.

Watumishi waliokoma utumishi kwa sababu ya kufukuzwa kazi 2,Watumishi walioghushi vyeti 3,Watumishi wenye kesi mahakamani 2

kwa mwezi Julai, 2017 Halmashauri ililipa kiasi cha Tsh 1,131,676,250/= kwa watumishi 1781 kati ya hao, watumishi 1760 wamelipwa Tsh 1,126,692,900 kwa ruzuku toka serikali kuu na watumishi 21 wamelipwa Tsh 4,983,350/= kwa ruzuku ya mapato ya ndani. Kati ya watumishi 21 watumishi 17 ni wa mkataba na watumishi 4 ni ajira ya kudumu

MUHT. NA.FUM/42/2017/2018 - TAARIFA YA KIKAO CHA BODI YA AJIRA

Ilielezwa kuwa, taarifa ya kikao cha Bodi ya Ajira kilichokaa tarehe 25/08/2017 kwa ajili ya kusaili wasaidizi wa hesabu pamoja na madereva wa mkataba. Taarifa ilipokelewa na wajumbe walishauri kuwa taratibu za kuajiri ziendelee.

D: KIKAO MAALUM CHA TAREHE 27/09/2017

MUHT. NA. FUM/45/2017/2018 - KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA YA UFUNGAJI WA HESABU ZA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Taarifa ilihusisha mchanganuo wote wa mali na madeni, mtiririko wa kifedha, hali ya utekelezaji wa kifedha na ulinganifu wa mapato na matumizi ya Halmashauri.

TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI HADI SEPTEMBA), 2017/2018

Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ilifanya kikao chake cha robo ya kwanza tarehe 30/10/2017 na kupitia taarifa za utekelezaji za Idara na vitengo vyake kwa robo ya kwanza.

MUHT NA. BM/38/2017/2018 – KUFUNGA KIKAO

Katibu aliwapongeza wajumbe kutokana na agenda mbalimbali walizochangia kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano walioonesha kupitia taarifa mbalimbali hadi kufikia mwisho wa taarifa zilizokuwa zimewasilishwa aliongeza kuwa ili kufanya vikao kuwa rahisi ni vyema mambo yote yaliyoagizwa kutekelezwa. Aliongeza kuwa kwa kuwa msimu huo ni wa kilimo wawakilishi wakawasisitize wananchi kujikita zaidi katika kilimo na wataalam hasa maafisa ugani wasikae ofisini waelekee shambani kuwashauri wakulima.

Aidha alimkumbusha Mkurugenzi Mtendaji kuwa, kuna changamoto ya upungufu mkubwa wa watendaji hali inayopelekea kazi nyingi kukwama hata taarifa za utekelezaji ngazi ya kata zimeshindwa kuwasilishwa. Pia aliomba jeshi la polisi lifanyie kazi malalamiko yaliyowasilishwa na waheshimiwa Madiwani kutokana na manyanyaso wanayofanyiwa wananchi.

Alifunga kikao saa 8:06 Mchana

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA

NA

SAINI: ..... **SAINI: .....**

JINA: ..... **JINA: .....**

CHEO: KATIBU **CHEO: MWENYEKITI**

.....

TAREHE